

Fomu fupi ya Kuridhia Kushiriki Utafiti

Unaombwa kushiriki mtaala wa utafiti. Kabla ya kuridhia kwako kuanza masomo, ni muhimu kwamba utapata maelezo wazi kuhusu masomo kwa lugha ambayo unaweza kufahamu. Jambo linalofuata ni orodha ambayo utakubali nayo ukitia sahihi kwenye fomu hii ya kuridhia.

Mfasiri ambaye ni mmoja wa watafiti wanaoongoza masomo ama ni mmoja wa wakilishi wao alikuelezea kuhusu (1) nia ya utafiti, utaratibu, na muda ambao utafiti utaendelea; (2) utaratibu wowote ulio wa majaribio; (3) hatari zozote za akili zinazojulikana mbele (hatari zinazowezezana zinazojulikana wakati huu), adha na faida za utafiti; (4) utaratibu wowote mwingine wa faida unaowezezana au jinsi ya kutenda; na (5) jinsi siri zitakazoendelezwa.

Uliponyeshwa masomo haya, ulikuwa umeambiwa kuhusu (1) fidia zozote zilizopatikana au utabibu ukiumizwa unapofanya utafiti; (2) uwezekano wa hatari zisizojulikana mbele (hatari zisizojulikana wakati huu); (3) kwa hali ilivyo mtafiti anaweza kumaliza kushiriki kwako (4) gharama zozote zinazoongezwa kwako; (5) zitakazotokea ukiamua kumaliza kushiriki; (6) utakapoambiwa matokeo mapya yangeathiri upendo wako kushiriki; na (7) watu wangapi watakuwa kwenye masomo.

Ulikuwa umeambiwa kwamba ukiumizwa kutokana na kuwa katika masomo haya ya utafiti, mara utapata utabibu wa lazima. Walakini, hakuna sharti kwa Wayne State University na washiriki wake kutoa fidia za fedha au utabibu bure kwako kutokana na dhara iliyohusika na masomo.

Ulikuwa umeambiwa unaweza kuwasiliana na _____, Mtafiti Mkuu (PI) kwa _____, ukiwa na maswali au matatizo kuhusu masomo na Ofisi ya Kamati ya Uchunguzi wa Watu kwa 313-577-1628 ukiwa na maswali yoyote kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti, masomo ya utafiti, au kufanya nini ukiumizwa.

Ulikuwa umeambiwa kwamba kushiriki kwako katika utafiti huu ni kwa hiari na kwamba hutatiwa hatiani ama hutapoteza faida ukikataa kushiriki au kuamua kumaliza baada ya kuridhia kwako kushiriki.

Ukikubali kushiriki, ulikuwa umeambiwa kwamba utapata nakala iliyotiliwa sahihi ya hati hii na muhtasari iliyoandikwa kuhusu utafiti kwa lugha ya Kiingereza.

Kutia sahihi hati hii kunamaanisha kwamba masomo ya utafiti, pamoja na taarifa iliyoandikwa hapo awali, yamekuelezwa kwa maneno, na kwamba unakubali kwa hiari kushiriki.

Sahihi ya Mshiriki/Mwakilishi wa kisheria Mwenye Mamlaka/Uhusiano

Tarehe

Sahihi ya shahidi

Tarehe

Sahihi ya mfasiri

Tarehe